

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

AnwaniyaSimu: "UCHUNGUZI"
SimuNambari: 262323315
Nukushi: 26232332
BaruaPepe: dgeneral@pcc.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz
Unapojibutafadhalitaja:



Mtaa wa Jamhuri,
S. L. P 1291,
41101 DODOMA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

IMETOLEWA JIJINI DODOMA
SEPTEMBER 16, 2022

TAKUKURU YACHAMBUA MFUMO WA USIMAMIZI WA
FEDHA ZA MAENDELEO YA MPIRA WA MIGUU
TANZANIA

TAKUKURU imefanya kikao kazi na wadau mbalimbali, kilichojadili matokeo ya 'Uchambuzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Maendeleo ya Mpira wa Miguu kwenye Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini – TFF', kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa inayoweza kujitokeza katika eneo hilo.

Kikao kazi hiki kimefanyika Septemba 15, 2022 katika Hoteli ya Rafiki jijini Dodoma, kwa kuishirikisha TAKUKURU na wadau mbalimbali kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Shirikisho la Mpira wa Miguu - TFF; Baraza la Michezo Tanzania – BMT pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA.

Akifungua kikao kazi hiki, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU CP. Salum Rashid Hamduni amesema uchambuzi uliofanyika umefanyika kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu cha 7(a) na (c)

cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Katika maelezo yake, amesema ustawi wa Maendeleo ya Mpira wa Miguu, hauwezi kufanikiwa bila kuhahikisha tunaimarisha usimamizi wa fedha za maendeleo ya Mpira wa Miguu na katika sekta ya michezo. Aidha, amewataka washiriki wa kikao kazi kushiriki kikamilifu katika mjadala na kuwa tayari kutekeleza mapendekezo ya mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa katika usimamizi wa fedha za maendeleo ya mpira wa miguu pamoja na sekta ya michezo kwa ujumla.

Awali, akitoa maelezo ya utangulizi, Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa TAKUKURU, Bi. Sabina Seja alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa – UNCAC na inatekeleza maazimio ya mkataba huo ya kuzuia na kupambana na rushwa katika sekta ya michezo.

Akitoa mchango wake wakati wa majadiliano, mwakilishi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Bw. Rashid Mijuzi ambaye pia ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa majadiliano hayo, alisema anaipongeza TAKUKURU kwa kufanya uchambuzi na kuitisha kikao kazi hiki ambacho amesema ni cha manufaa katika mustakabali wa maendeleo ya mpira wa miguu nchini.

IMETOLEWA NA:



DOREEN J. KAPWANI

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
TAKUKURU**